JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Chuo cha Ualimu Tandala,

Anuani ya Simu: Mkuu wa chuo
Simu: 0752-716257
Msajili: 0763086245

S.L.P.377,
NJOMBE.

Barua pepe: tandalatc@gmail.com

03/07/2020

Kumb.Na TTC/UW/17/48

Ndugu ……
……
……

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU MGAZI YA STASHAHADA ELIMU YA MSINGI/AWALI 2020/2021.

UTANGULIZI

Unapongezwa kwa kuchaguliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kujiunga na mafunzo ya Ualimu ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Msingi/Awali (Diploma) katika Chuo cha Ualimu Tandala. Muda wa mafunzo ni miaka miwili (03).

MAHALI CHUO KILIPO NA NAMNA YA KUFIKA

Chuo kipo katika kijiji cha Tandala Wilayani Makete (Mkoa wa Njombe) umbali wa kilometa 86 toka Njombe. Ukifika Njombe panda mabasi yanayoelekea Ikonda, kama utafika jioni baada ya mabasi yanayoelekea Ikonda-Makete kuondoka, uliza nyumba za kulala wageni zilizopo karibu na stendi kwenye ofisi za mabasi.

Ukifika Ikonda telemka katika kituo cha mabasi ulizia sehemu Chuo kilipo, umbali wa kutoka Ikonda hadi chuoni ni kilomita moja ambapo unaweza kutembea kwa miguu.

Dira ya Chuo

Kutoa walimu mahiri wa Stashahada (Diploma) wenye maarifa, ujuzi na stadi wanaoweza kukabiliana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na changamoto mbalimbali za maisha kisiasa, kijamii na kiuchumi. Moto wa Chuo ni "**Elimu ni Kazi"**

MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI

- **VIFAA VYA DARASANI**
    - Ream moja ya karatasi ya A.4. (Photocopy) kwa ajili ya mazoezi na mitihani ya ndani kila mwaka (**zinapatikana maduka ya karibu na chuo).**
    - Daftari 20 size ya (Four au three Quire) kwa masomo utakayosoma.
    - Mathematical set 1
    - Kalamu za wino, penseli na rula ndefu.
    - Mkoba nadhifu wa kuchukulia daftari,na vitabu. ***Ni marufuku*** kwa mwanachuo kuweka daftari, vitabu, rula katika mfuko wa suruali, sketi, katika nguo ulizovaa au mkononi. Mifuko ya plastiki, viroba na vingine visivyo vya hadhi ya mwalimu ni marufuku darasani.

- **VIFAA VINGINE**

Uwe na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi yako binafsi.

- Bakuli na sahani za bati (siyo plastiki), kijiko, na uma kwa ajili ya kulia chakula na ndoo ya ujazo wa lita 20 kwa ajili ya usafi binafsi.
- Mablanketi mazito mawili, shuka mbili za **pink kwa wasichana** na **bluu bahari kwa wavulana** pamoja na mto wenye foronya unaofanana na rangi ya shuka. Shuka za rangi nyingine hazitaruhusiwa.
- Nguo za michezo aina ya track suit rangi ya kijivu au nyeusi za dukani zisizo na kofia na siyo mtumba.
- Bukta na fulana za rangi nyekundu au njano na raba za michezo za rangi mbalimbali.

- **SARE**

Wasichana

- Shona suti nyeusi (sketi iwe kama mchoro namba 1 unavyoonesha).
- Shati la light blue mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi/kawaida.
- Soksi nyeupe.
- Tai nyeusi sio “neck tie”
- Kwa wanachuo waislam wanaruhusiwa kuvaa hijab nyeupe.

PICHA 1



Wavulana

- Shona suti nyeusi (suruali iwe kama mchoro namba 2 unavyoonesha)
- Shati la light blue mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi/kawaida.
- Soksi nyeusi.
- Tai nyeusi sio “neck tie”

PICHA 2



* **Mavazi ya mitumba na mishono ambayo hayajaelekezwa hayatapokelewa**

- **MAVAZI MENGINE**
  - Leta mavazi ya heshima ya kiualimu.
    Kwa wasichana: sketi au gauni fupi **halitakiwi**. Sketi au gauni lenye kubana mwili au kuonekana limegeuzwa au kuangaza halitakiwi.
    Kwa wavulana: aina ya jinsi, dengriz ama suruali za kupandisha mpaka tumboni au kushusha chini ya kiuno hazitakiwi.
  - **Nywele:** kwa wasichana nywele za bandia hazitakiwi, kwa wavulana hutakiwi kunyoa kipara au mitindo yoyote ya kihuni, masweta au makoti yawe ya heshima.
- **ADA**
  - Ada ni shilingi laki nne na elfu hamsini (450,000/=) kwa mwaka.
  - Nusu mwaka (muhula mmoja) ni Tshs 225,000/=
  - Kulipa karo ni lazima bila karo na michango mingine hutapokelewa. Wazazi/walezi wa wanachuo mnatakiwa kulipa ada ya Chuo kupitia namba maalumu (cotrol number) ambayo mtapewa na Mhasibu wa chuo mara tu mfikapo chuoni (Au waweza wasiliana na mhasibu kwa namba 0767-285709) ili upewe control number).

- **MICHANGO MINGINE**
  - Huduma ya kwanza (Tshs 10,000/= kwa mwaka.
  - Usajili na kitambulisho Tshs 20,000/=inalipwa mara moja mwaka wa kwanza tu.
  - Serikali ya wanachuo 5,000/=kwa mwaka.
  - Elimu ya michezo Tshs 30,000/= kwa mwaka.
  - Ulinzi Tshs 30,000/= kwa mwaka
  - Usafi, mazingira na EK Tshs 20,000/=kwa mwaka
  - Ukarabati Tshs 25,000/=kwa mwaka
  - Kukodi godoro Tshs 10,000/= kwa mwaka.

Fedha za michango yote iliyotajwa (i)-(viii) hapo juu zinatakiwa ziwekwe kupitia Benki ya NMB kwenye Akaunti ya Chuo iitwayo **"TANDALA TEACHERS COLLEGE" NAMBA 60401100008 NMB** ambayo imefunguliwa na Serikali.
N.B: Chuo hakitapokea fedha taslim kutoka kwa wanachuo kwa sababu zozote zile. Aidha kila mwanachuo anatakiwa kuja na BANK-PAY-IN SLIP halisi toka bank sio nakala (photocopy) na ziwe na jina kamili la mwanachuo. **Fedha zikishaingizwa kwenye akaunti ya Serikali ya NMB hazitarudishwa.**

- **KABLA YA KUFIKA CHUONI**

Nenda kwa daktari anayetambuliwa na Serikali ili upimwe afya yako, fomu ya kupima afya imeambatanishwa. **Chuo hakina huduma maalumu ya chakula na matibabu kwa wagonjwa, endapo una bima itagharamia matibabu yako.**

- **UTAMBULISHO**

Unatakiwa kuja na **vyeti halisi (siyo nakala/vivuli)** vifuatavyo:-

- Cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving Certificate) chenye picha na mhuri wa Mkuu wa Shule uliogongwa juu ya picha yako katika cheti chako/Result slip.
- Cheti cha matokeo ya mitihani ya kitaifa cha Baraza la Mitihani ya kidato cha nne yaani Academic Certificate.
- Cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) ni lazima ulete, majina yalingane na cheti cha NECTA.

Kutoleta vyeti vilivyotajwa hapo juu kutafanya **USIPOKELEWE. Kuleta vyeti vya bandia au ambavyo sio vyako ni uvunjaji wa sheria za nchi (hatia) ukibainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.**

- **MAPOKEZI**

Mara ufikapo chuoni fika Ofisi ya Usajili kwa utambulisho na kukabidhi vyeti, risiti za benki za ada na michango, na vifaa mbalimbali.

Pamoja na maelezo ya hapo juu, kama upo tayari kusoma katika Chuo hiki utatakiwa kufuata kanuni za Chuo. Ukifika chuoni utapitishwa katika taratibu za Chuo aidha, utapewa fomu ya kujaza kukubaliana na sheria na kanuni za Chuo. Ukivunja kanuni hizo utaondolewa chuoni.

MWISHO

Tarehe ya kuripoti ni 01/10/2020 ifikapo tarehe 14/10/2020 hutopokelewa.

KARIBU CHUO CHA UALIMU TANDALA

NATHANAEL A.HINJU
MKUU WA CHUO

Nakala: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10,

DODOMA.

Mkaguzi Mkuu.
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini,
S.L.P. 2288,
IRINGA

Afisa Elimu,
Mkoa wa Njombe,
S.L.P. 858,
NJOMBE

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo,
S.L.P. 1,
MAKETE.

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

PART A:

To: The Medical Officer,

……. From……
……. Teachers' College

Please Examine the above named as to him/her physical and mental fitness for a full time Teachers Course.

A:1

- Eye – Sight
- Hearing
- Speech
- Venereal diseases
- Leprosy
- Limbs
- Epilepsy

2. Neuroses
3. Other serious diseases

B: Blood Group

Date: …… Signature ……

Official Stamp

****

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally fit /unfit for a full time teacher Education course.

I. (a) Eye - Sight…….
(b) Hearing…….
© Limbs…….
(d) Speech……..
(e) Leprosy …….

II. Neuroses ……

III. Other serious disease…….....

IV.Pregnancy……..

Date: …….. Signature ……

Official Stamp